AFP

# Mwingiliano wa Kigeni katika Jumuiya

Jinsi ya kutoa taarifa ya vitisho na kuogofywa kutoka serikali za kigeni

FACTSHEET / March 2023

afp.gov.au

## Utangulizi

Mwingiliano wa kigeni unakuwa tishio kubwa kwa watu, enzi kuu na usalama wa Australia, na uaminifu wa taasisi zetu za kitaifa. Matisho ya mwingiliano wa kigeni hayazuiliwi na sekta moja ya jumuiya ya Australia na hayafanywa kosa na serikali na taifa moja pekee. Wahusika wenye uadui wa serikali za kigeni (yaani nchi ambazo zinafanya shughuli za uhasama dhidi ya nchi nyingine) wanaunda na kutafuta fursa za kuingilia kati ya waamuzi wa Australia wa viwango vyote vya serikali na kote sekta mbalimbali, ikiwa pamoja na: sheria na desturi za kidemokrasi za kawaida; elimu na utafiti; vyombo vya habari na mawasiliano; miundombinu muhimu; na muhimu, jumuiya tofauti zetu za kitamaduni na kiisimu (CALD).

## Mwingiliano wa kigeni katika jumuiya

Mwingiliano wa kigeni katika jumuiya unafafanuliwa kama matisho na kuogofya ambayo yameongozwa, kusimamiwa au kufadhiliwa na serikali za kigeni na yanayolengwa kwa jamii za CALD ili kusababisha madhara na athari kwa njia ya maisha ya tamaduni nyingi ya Australia. Serikali za kigeni zinaweza kuingilia kati ya jamii kwa makusudi mbalimbali:

- kunyamazisha ukosoaji wa sera za serikali ya kigeni za ndani na nje
- kufuatilia shughuli (nje mtandaoni na mtandaoni) za wanachama wa vikundi vya CALD
- kukuza maoni na sera za serikali ya kigeni
- kupata taarifa kwa faida ya serikali ya kigeni
- kuathiri maoni na mawazo ya idadi kubwa ya watu.

## Mwingiliano wa kigeni katika jumuiya unaweza kuwa aina nyingi

Ikiwa ni pamoja na:

- Shambulio au matisho ya shambulio
- Usaliti
- Utekaji nyara, kufunga kwa haramu au kunyima uhuru.
- Kuwinda na upelelezi usiotakiwa wa kimwili au kielektronik
- Kulazimisha mtu binafsi kwa kuwatisha jamaa wake au wenzake wa nje ili kumlazimisha kutii
- Kampeni mtandaoni za taarifa za uongo kupitia mtandao wa kijamii ili kupunguza sifa ya mtu au kikundi.

Muhimu, ili itambuliwe kuwa mwingiliano wa kigeni chini ya Sheria ya Kanuni ya Jinai 1995 (Cth), shughuli inapaswa kuunganishwa na serikali ya kigeni au wakala wake. Katika kutathmini uhalifu, mashirika ya kutekeleza sheria yanaweza pia kuzingatia makosa ya Jimbo na Wilaya ya Australia.

## Nani analengwa?

Serikali za kigeni zinaweza kulenga:

- Raia zao wa zamani au wa sasa wanaoishi nchini Australia
- Wanaharakati wa kisiasa na wa haki za binadamu
- Wapinzani
- Waandishi wa habari
- Wapinzani wa kisiasa
- Makundi madogo ya watu wa kidini au kikabila.

## Je, niweze kufanya nini kusaidia?

Ingawa sio ripoti zote za mwingiliano wa kigeni katika jumuiya zitatoa jibu dhahiri ya AFP, kila ripoti **husaidia kuonyesha picha** ya masuala yanayojitokeza.

Wasiwasi wowote na/au matukio ya mwingiliano wa kigeni katika jumuiya yanaweza kuripotiwa kwa **Simu Muhimu ya Usalama wa Kitaifa** (**National Security Hotline) (NSH)**.

- NSH hufanya kazi masaa 24 za siku, siku 7 za wiki na ndio sehemu kuu ya mawasiliano ya kuripoti masuala kuhusu uwezekano wa kuingiliwa na mataifa ya kigeni katika jumuiya.
- Waendeshaji simu wa NSH watajua la kufanya na taarifa unayotoa, na anapofaa, watatoa taarifa kwa vyombo vya kutekeleza sheria na vyombo vya usalama kwa ajili ya tathmini.
- Waendeshaji simu wa NSH wanachukua kwa uzito kila simu na wanathamini habari zote zilizopokelewa.
- Tunajua kwamba kuripoti jambo la kuhangaisha inaweza kuwa hatua kubwa. Tunachukua kwa uzito haki yako ya faragha. Tafadhali umwambie mwendeshaji simu ikiwa ukitaka kutokujulikana.
- Kutokana na hali nyeti ya habari, hutapokea ushauri kuhusu matokeo ya simu au barua pepe yako.

Taarifa unazozipokea zinaweza kuwa kipande kilichokosekana ambacho AFP kinahitaji ili kuzuia mwingiliano wa kigeni katika jumuiya.

Kuna njia chache za kuwasiliana na **NSH:**

- **Piga simu: 1800 123 400**
  - Kutoka nje ya Australia: (+61) 1300 123 401
  - Kwa watumiaji wa TTY (watumiaji wenye ulemavu wa kusikia): 1800 234 889
  - **Ikiwa unahitaji mkalimani, tafadhali piga simu kwa Huduma ya Utafsiri na Ukalimani kwenye 131 450 na umwulize kupiga simu kwa Simu Muhimu ya Usalama wa Kitaifa**
- **SMS**

- Tafadhali tuma maelezo yako kupitia ujumbe ya maandishi kwa 0498 562 549

- **Barua pepe**
  - Tafadhali tuma maelezo yako kupitia barua pepe kwa: hotline@nationalsecurity.gov.au
- **Tuma kwa posta:**
  - Tafadhali tuma kwa njia ya posta maelezo yako kwa:

    National Security Hotline
    Department of Home Affairs
    PO Box 25
    Belconnen ACT 2616

## Njia nyingine za kutoa ripoti

Unaweza pia kutoa ripoti wasiwasi wako kupitia anuwai ya njia nyingine zinapofaa.

- eSafety husaidia kuondoa maudhui ya mtandaoni yenye matusi makubwa. Unaweza kutoa taarifa ya matusi makubwa ya mtandaoni kwa Kamishna wa eSafety kwa esafety.gov.au/report.
- Ikiwa unajisikia **kutishwa au kutokuwa salama** kwa njia yoyote**,** unaweza kuwasiliana na**:**
  - **Polisi - kwa 000 kuhusu vitisho vya haraka**
  - **Polisi - kwa 13 14 44 ili polisi wahudhurie kwenye matukio yasiyo ya kutishia maisha.**
- Unaweza kutoa taarifa ya jinai ya Taifa kwa AFP kupitia fomu mtandaoni Toa Ripoti kuhusu Jinai ya Taifa kwa forms.afp.gov.au/online_forms/report_a_crime. Kupata maelezo zaidi juu ya ni nini maana ya Jinai la Taifa, tafadhali ona kwa afp.gov.au/contact-us/report-commonwealth-crime#What-is-a-Commonwealth-crime.
- Mtu yeyote wa jumuiya anaweza kuripoti shughuli za ujasusi unaoshukiwa au mwingiliano wa kigeni kwa kuzungumza moja kwa moja na mwanachama wa AFP (akiwemo Timu ya Uhusiano wa Jamii ya AFP).

## Je, ni nini naweza kutarajia kwa kutoa taarifa juu ya mwingiliano wa kigeni katika jumuiya?

AFP haiwezi kuchunguza kila ripoti ya mwingiliano wa kigeni katika jumuiya. Kila simu kwa NSH au taarifa ya jinai katika kila kesi ili kuamua kama kosa lolote la jinai linatambuliwa. Matokeo ya kutoa taarifa yanajumuisha:

- kunaweza kuwa hakuna jibu kwa sababu jambo haliridhi kiwango cha juu cha kisheria kwa polisi kuchukua hatua
- AFP inaweza kuchunguza
- shirika lingine la polisi au la serkali linaweza kushughulikia jambo.

Kwa makosa ya jinai yanayotokea nje ya Australia, mipaka ya mamlaka inatumika.

# Aina za matisho

## Ikiwa unatishiwa kibinafsi

- Andika au fanya kumbukumbu ya tishio halisi kama lilivyowasilishwa.
- Rekodi vitu vingi vya maelezo kuhusu mtu aliyefanya tishio (jina, jinsia, urefu, uzito, rangi ya nyewele na macho, sauti, nguo au sehemu muhimu tofauti yoyote nyingine).
- Toa taarifa ya tishio kwa polisi.

## Ikiwa unatishiwa kupitia simu

- Ikiwezekana, ashiria wengine walio karibu wasikilize na kuwaarifu polisi.
- Rekodi simu ikiwezekana.
- Andika maneno halisi ya tishio.
- Fanya nakala ya taarifa yoyote ya maonyesho ya kielektroniki ya simu.
- Upatikane kuzungumza maelezo na polisi.

## Ikiwa unatishiwa kupitia njia za kielektroniki ikiwa ni pamoja na kupitia ujumbe wa maandishi, ujumbe wa moja kwa moja/faragha, mtandao wa kijamii au barua pepe

- Usifute ujumbe.
- Chapisha, piga picha, piga picha ya skrini, au fanya nakala ya maelezo ya ujumbe (mstari wa mazungumzo, tarehe, saa, mtumiaji, n.k.). Hakikisha uhifadhi au upige picha ya skrini ya ujumbe ambao umekusudiwa kuwa wa muda tu.
- Mara moja uwaarifu polisi kwamba umetishiwa.
- Hifadhi ushahidi wote wa kielektroniki.

**Kujilinda kutoka aina hizi za matishio, fuata ushauri huu:**

- **Usifungue ujumbe wa kielektroniki au viambatisho kutoka wapelekaji wasiojulikana**
- **Usiwasiliane kwenye mtandaoni wa kijamii na watu binafsi wasiojulikana au bila kuombwa**
- **Hakikishe kwamba mipangilio yako ya usalama kwenye vifaa/akaunti zako imewekwa kiwango cha juu sana cha ulinzi**
- **Wahalifu wa mtandaoni wanaweza kutia matatani vifaa vyako vya kielektroniki na kufichua maelezo ya kibinafsi**
- **Mara moja wasiliana na taasisi zako za kipesa ili kulinda akaunti zako kuzuia wizi wa utambulisho**
- **Tumia maneno ya siri yenye nguvu na usitumie maneno ya siri yale yale kwa tovuti nyingi**
- **Hakikisha programu za kuzuia virusi na kuzuia malware ni za sasa hivi**
- **Tumia sasaisho za mfumo na programu zinapohitajika**
- **Tumia uhalalishaji wa njia mbili**
- **Hifadhi nakala za data kila mara**
- **Funga kifaa chako cha mkononi**
- **Ongeza mawazo yako na ufahamu wako wa Usalama wa Mtandanoi (Cyber Secure)**
- **Kwa habari zaidi, tembelea kwa cyber.gov.au.**